**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# MWONGOZO WA UENDESHAJI WA VITUO VYA KUTOA HUDUMA ZA ZANA ZA KILIMO



**WIZARA YA KILIMO**
**DODOMA-TANZANIA**
**JULAI, 2025**

## DIBAJI



Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuimarisha usalama wa chakula na lishe pamoja na maendeleo ya Sekta ya viwanda kwa ujumla.

Serikali imeendelea kuandaa miongozo na mikakati mbalimbali ili kuongeza kasi katika kukuza Sekta ya Kilimo lengo likiwa ni kufikia ukuaji wa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Pamoja na mambo mengine ukuaji wa Sekta ya Kilimo unaathiriwa na uzalishaji wa mazao chini ya viwango vya tija vinavyopendekezwa na utafiti, mfano wastani wa uzalishaji wa alizeti katika Kanda ya Kati ni tani 1.2 kwa hekta ikilinganishwa na uwezekano wa kuzalisha tani 4.0 kwa hekta. Uzalishaji na tija wa chini ya kiwango pamoja na mambo mengine unachangiwa na matumizi yasiyoridhisha ya zana za kilimo. Wakulima wengi hawatumii zana za kilimo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo; uhaba wa zana hizo katika maeneo yao, uwezo mdogo wa kifedha wa wakulima walio wengi kugharamia ununuzi wa zana hizo, pamoja na kukosekana kwa vipuri na utaratibu mzuri wa kutoa huduma za zana za kilimo.

Ili kutatua changamoto za matumizi ya zana za kilimo kwa wakulima hususan wadogo, Serikali inawekeza kwenye uanzishwaji wa Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo ambavyo vitatoa huduma katika mnyororo mzima wa thamani ya mazao ya kilimo kulingana na mahitaji ya wadau. Hivyo, mwongozo huu unaweka utaratibu wa kuanzisha na kutoa huduma za zana za kilimo na utatumiwa na wadau wote wa Sekta ya Umma na Binafsi waliopo

katika mnyororo huo, wakiwemo Maafisa ugani kilimo, mafundi sanifu zana za kilimo, maopereta na watendaji wengine ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji, matengenezo na utunzaji wa zana za kilimo. Hatua hiyo itawezesha kuongeza matumizi ya zana za kilimo kwa wakulima na kuongeza uzalishaji na tija.

Ninapenda kuchukua nafasi hii kusisitiza kuwa, Mwongozo huu ni mojawapo ya jitihada ya kuhakikisha Serikali inafikia malengo na shabaha iliyojiwekea katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi; Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa; Ajenda 10/30, Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo Tanzania 2050 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030. Nitoe rai kwa wadau wote kuzingatia maelekezo yaliyomo katika mwongozo huu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Hussein M. Bashe (Mb)
**WAZIRI WA KILIMO**

## SHUKRANI



Serikali inatambua umuhimu wa matumizi ya zana za kilimo katika kuleta mageuzi kwenye Sekta ya Kilimo nchini. Matumizi ya zana za kilimo yataongeza eneo linalolimwa, ufanisi wa shughuli za kilimo na kupunguza harubu zilizopo katika kazi za kilimo.

Vilevile, Serikali kwa kutambua changamoto zilizopo katika matumizi ya zana za kilimo hususan kwa wakulima wadogo, imefanya uwekezaji mkubwa kwa kuanzisha vituo vya kutoa huduma za zana hizo. Vituo hivyo, vitasimamiwa na Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na Sekta binafsi ili viwe endelevu na kuleta tija kwenye mapinduzi ya kilimo.

Aidha, Mwongozo wa uendeshaji wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo umeandaliwa ili kuwa na ufanisi wa utendaji katika vituo hivyo. Mwongozo huu, unaweka utaratibu wa kutoa huduma za zana za kilimo na kuhakikisha vituo vilivyoanzishwa na vitakavyoanzishwa vinatoa huduma iliyokusudiwa kwa njia endelevu. Pia, utasaidia kuwaunganisha wadau katika kuanzisha, kuendesha na kusimamia vituo hivyo.

Usimamizi madhubuti na endelevu wa Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo utawezesha na kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuongeza ajira. Hata hivyo, ili kuendana na mahitaji ya watumiaji wa huduma za zana za kilimo nchini, Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kadri itakavyoonekana inafaa.

Mwongozo huu, umeandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Umma na Binafsi ambao wameshiriki kikamilifu katika kutoa maoni yaliyosaidia kukamilisha Mwongozo huu. Kwa muktadha huu, ninawashukuru wadau wote kutoka Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Sekta Binafsi walioshiriki katika kazi ya kuandaa Mwongozo. Ninatoa shukrani za dhati kwa Menejimenti na watumishi wa Wizara ya Kilimo kwa kazi ya kuratibu wadau na kukamilisha mwongozo huu.

Gerald G. Mweli, *ndc*
**KATIBU MKUU**

## MAANA YA MANENO

1. **Karakana:** Eneo maalum linalotumika kufanya matengenezo ya zana mbalimbali za kilimo.

2. **Mashine za kilimo:** Zinahusisha zana kama trekta kubwa; trekta za mikono; mashine za kukata; mashine za kuvuna; mashine za kupura; mashine za kusindika; vifaa vya miundombinu ya uhifadhi.

3. **Mkulima mdogo:** Katika Mwongozo huu, mkulima mdogo ni mkulima anayemiliki eneo lisilozidi ekari 50 na anayejishughulisha na shughuli za kilimo.

4. **Nguvu kazi**: Nguvu inayotumika katika kutenda kazi ikiwemo binadamu; wanyama kazi na mashine

5. **Zana za kilimo:** Teknolojia mbalimbali zinazotumika katika mnyororo wa uzalishaji wa mazao ya kilimo kupitia matumizi ya zana za mikono, viambata, mashine, miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa mazao.

6. **Zana za mikono:** Zana zinazotumika kwa mikono kama vile jembe la mkono, panga, mundu, shoka, reki, fyekeo

7. **Viambata:** Zana zinazotumika kwa kuunganishwa kwenye mashine za kilimo kama vile jembe la sahani, jembe la kucha, haro, ripa, jembe tindo, kipandio, jembe la palizi, jembe la kuchavanga, tela za kubebea mizigo.

8. **Vituo vya Zana za kilimo:** Vituo jumuishi vilivyoanzishwa au vitakavyoanzishwa mahususi kutoa huduma ya kukodisha zana, kukarabati zana chakavu za kilimo, kutoa ushauri na kufundisha matumizi bora ya zana za kilimo vikijumuisha wataalamu wa mashine za kilimo, rasilimali watu na

wataalamu wa fedha.

9. **Watoa huduma za zana za kilimo:** inahusisha wakodishaji binafsi wa zana za kilimo, watengenezaji wa zana za kilimo, wauzaji wa vipuri na mafuta.

# YALIYOMO


**DIBAJI** ........ i

**SHUKRANI** ........ iii

**MAANA YA MANENO** ........ v

**1.0 UTANGULIZI** ........ 4

- **1.2 Mamlaka ya Wizara ya Kilimo katika kuandaa Mwongozo** ........ 5
- **1.3 Juhudi za Serikali za kuendeleza Zana za Kilimo Nchini** ........ 5
- **1.4 Hali ilivyo sasa ya Matumizi ya Zana za Kilimo** ........ 8
- **1.5 Chimbuko la Mwongozo** ........ 9
- **1.6 Walengwa wa Mwongozo** ........ 10
- **1.7 Malengo ya Mwongozo** ........ 10
  - **1.7.1 Lengo Kuu** ........ 10
  - **1.7.2 Malengo Mahsusi** ........ 11
- **1.8 Mantiki ya Mwongozo** ........ 11

**2.0 UTARATIBU NA VIGEZO VYA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA ZANA ZA KILIMO KATIKA VITUO VYA SERIKALI** ........ 12

- **2.1 Utaratibu wa Usimamizi wa Vituo vya Serikali** ........ 12
  - **2.1.1 Muundo wa Usimamizi** ........ 13
  - **2.1.2 Mgawanyo wa Majukumu** ........ 13
- **2.2 Majukumu ya Wizara ya Kilimo** ........ 13
  - **2.2.1 Majukumu ya Idara ya Zana za Kilimo na Uongezaji Thamani** 14
  - **2.2.2 Majuku ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa** ........ 15
  - **2.2.3 Majukumu ya Mamlaka ya Srikali za Mitaa** ........ 16
  - **2.2.4 Majukumu ya wasimamizi wa Vituo vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo** ........ 16
  - **Wasimamizi wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo kwa wakulima watakuwa na wajibu ufuatao;** ........ 16
  - **2.2.5 Vigezo vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo** ........ 17
  - **2.2.6 Sifa za Waombaji wa Huduma za Zana za Kilimo** ........ 18

2.2.7 Hali ya Shamba .......... 18
2.2.8 Vyama vya Ushirika/Umoja/Vikundi vya Wakulima/Kampuni 19
2.2.9 Modeli ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Serikali ...... 19

2.3 Majukumu ya Wadau Wengine .......... 20
2.3.1 Ofisi ya Rais-TAMISEMI .......... 20
2.3.2 Wizara ya Fedha .......... 20
2.3.3 Taasisi za Kifedha .......... 21
2.3.4 Tume ya Maendeleo ya Ushirika .......... 21
2.3.5 Sekta binafsi .......... 21
2.3.6 Washirika wa Maendeleo .......... 22
2.3.7 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) 22
2.3.8 Vyombo vya Habari .......... 23

3.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UENDESHAJI WA VITUO VYA ZANA ZA KILIMO .......... 23

3.1 Ukokotoaji Mjengeko wa Gharama za Kutoa Huduma za Zana za Kilimo 24

3.2 Mchanganuo wa Matumizi ya Mapato .......... 25

3.3 Tathmini ya Maendeleo ya Vituo .......... 26

3.4 Ukaguzi wa Zana za Kilimo .......... 26

3.5 Matengenezo na Matengenezo Kinga .......... 27

3.6 Vipuri na Vilainishi .......... 27

3.7 Usalama wa Zana za Kilimo .......... 28

3.8 Opareta wa Zana za Kilimo .......... 28

3.9 Uondoshaji wa Zana za Kilimo katika Vituo .......... 28

4.0 MASUALA MTAMBUKA .......... 29

4.1 Jinsia, Vijana, Wazee na Watu wenye Mahitaji Maalum .......... 29

4.2 Mabadiliko ya Tabianchi na Utunzaji wa Mazingira .......... 29

4.3 Utawala Bora .......... 29

**5.0 UENDELEVU WA VITUO VYA KUTOA HUDUMA ZA ZANA ZA KILIMO ........ 30**

**5.1 Usimamizi na Matengenezo ya Zana za Kilimo ........ 30**

**5.2 Upatikanaji wa mafuta na vilainishi *(lubricants)* ........ 31**

**5.3 Usimamizi wa Fedha na Mapato ........ 31**

**5.4 Kuratibu mafunzo na tafiti za zana za kilimo ........ 33**

**5.5 Matumizi ya mifumo ya kidigitali ........ 33**

**5.6 Ushirikishwaji wa jamii ........ 33**

**5.7 Huduma ya matengenezo na mfumo wa kidigitali ........ 34**

**6.0 TARATIBU KWA VITUO VITAKAVYOENDESHWA NA WATOA HUDUMA BINAFSI ........ 34**

**6.1 Modeli ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Sekta Binafsi .. 34**

**6.1.1 Modeli ya ushirika/umoja wa wakulima ........ 35**

**6.1.2 Modeli ya Mkulima binafsi ........ 35**

**6.1.3 Modeli ya Kampuni binafsi ........ 35**

**7.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 35**

**8.0 MAPITIO YA MWONGOZO ........ 36**

# 1.0 UTANGULIZI

Pamoja na mambo mengine, Serikali imeendelea kuweka mkazo wa kuendeleza matumizi ya zana za kilimo kupitia Sera na mikakati mbalimbali ya Kitaifa inayolenga kuendeleza Sekta ya kilimo. Hata hivyo, pamoja na juhudi za Serikali za kuleta mabadiliko katika kilimo, matumizi ya zana za kilimo kwa wakulima wadogo yameendelea kuwa siyo ya kuridhisha ikilinganishwa na nchi zilizoendelea. Changamoto kubwa ni pamoja na gharama kubwa ya uwekezaji wa zana za kilimo, ukosefu wa uratibu wa wadau wanaotoa huduma za zana za kilimo kukidhi mahitaji ya wakulima, uelewa mdogo kuhusu faida za matumizi ya zana za kilimo, ukosefu wa Mwongozo na Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo na matengenezo ya zana za kilimo katika maeneo ya vijijini.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka dhamira ya uwekezaji wa trekta kubwa 10,000 na trekta ndogo za mkono (powertillers) 800 ili kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa huduma za zana za kilimo katika mnyororo wa uzalishaji mazao ya kilimo kulingana na mahitaji ya wadau hususan wakulima wadogo. Kwa kutambua uwekezaji mkubwa wa zana za kilimo unaoendelea kufanywa na Serikali, Wizara inaendelea na uanzishaji wa vituo 1000 vya Kata, Kanda na Taifa vya kutoa huduma za zana za kilimo katika mikoa mbalimbali nchini. Uwekezaji huu wa zana za kilimo, utaongeza uzalishaji, tija, ufanisi wa shughuli za kilimo, kuimarisha usalama wa chakula pamoja na maendeleo ya Sekta ya kilimo kwa ujumla.

Mwongozo huu, unaweka utaratibu wa kutoa huduma za zana za kilimo na kuhakikisha vituo vilivyoanzishwa na vitakavyoanzishwa vinatoa huduma iliyokusudiwa kwa njia endelevu. Pia, utasaidia kuwaunganisha wadau katika kuanzisha, kuendesha na kusimamia

vituo hivyo ili kuchochea na kuwezesha uzalishaji endelevu hususan kwa wakulima wadogo. Kipaumbele cha Serikali ni kuanzisha teknolojia shirikishi zinazokubalika kimazingira na kijamii na ambazo zinaweza kuchangia kuondoa umaskini pamoja na kuimarisha usalama wa chakula na lishe.

## 1.2 Mamlaka ya Wizara ya Kilimo katika kuandaa Mwongozo

Mwongozo wa uendeshaji Vituo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo umeandaliwa kwa kuzingatia Majukumu na Muundo wa Wizara ya Kilimo yaliyopitishwa na Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 04 Julai, 2022. Katika Muundo huo, Wizara ya Kilimo pamoja na majukumu mengine imepewa jukumu la kuandaa Sera, Mikakati na Miongozo ya matumizi bora ya zana za kilimo na umwagiliaji. Hivyo, maandalizi ya mwongozo huu ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanayohusu matumizi bora ya zana za kilimo.

## 1.3 Juhudi za Serikali za kuendeleza Zana za Kilimo Nchini

Kipindi baada ya uhuru, Serikali ilianzisha skimu 40 za makazi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo zana za kilimo hasa matrekta yalitumika kwa ajili ya kutayarisha na kulima mashamba. Zaidi ya asilimia 60 ya gharama ya uwekezaji wa Serikali katika skimu hizo za makazi ulikuwa ni kwa ajili ya matrekta na zana zake. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea na juhudi nyingine za kuhakikisha matumizi ya zana za kilimo yanaongezeka. Mwaka 1963, Serikali iliingiza nchini matrekta 159 ambayo yalitumiwa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika la Victoria (*Victoria Federation of Cooperative Union)* kwa lengo la kukodisha kwa wakulima katika mashamba makubwa ya pamba. Mchango mkubwa ulitolewa na Chama cha Wakulima (*Tanganyika Farmers Association*) ambapo kilisaidia kutoa mikopo kwa ajili ya kununua matrekta na zana zake

na mashine za kuvunia nafaka kwa ajili ya kukodisha kwa wakulima wa ngano na mahindi.

Vilevile miaka ya 1970, vituo vya kukodisha matrekta vya mikoa na wilaya vilianzishwa na mikopo nafuu ilitolewa kwa wakulima, vijiji vya ujamaa pamoja na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kununua matrekta na zana zake kupitia iliyokuwa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (CRDB) pamoja na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC). Pia katika kipindi hicho, kiwanda cha kutengeneza zana za kukokotwa na wanyamakazi kilichojulikana kwa jina la *Ubungo Farm Implement* (UFI) kilianzishwa. Kiwanda hicho, kilikuwa na uwezo wa kutengeneza majembe ya mkono 2,500,000 na plau zinazokokotwa na maksai 30,000 kwa mwaka. Mwaka 1972, Azimio la Iringa la Siasa ni Kilimo, lilielekeza Serikali kuongeza matumizi ya wanyamakazi ambapo vituo 80 vya kufundisha matumizi ya wanyamakazi *Oxenization Training Centers* (OTCs) vilianzishwa nchini kote. Hali hii, iliinua kwa kiasi kikubwa matumizi ya zana za kilimo kwani idadi ya matrekta yaliyokuwa yanatumika nchini ilifikia 9,000 mwaka 1975.

Mwaka 1981, Serikali ilianzisha Kampuni ya Kuunganisha Trekta aina ya Valmet (*Tanzania Tractor Manufacturing Company Limited-TRAMA*) ambayo ilikuwa na uwezo wa kuunganisha matrekta 300-500 kwa mwaka. Mwaka 1984, Serikali ilianzisha Kiwanda cha Zana za Kilimo (ZZK) katika mkoa wa Mbeya ambacho kilikuwa na uwezo wa kutengeneza majembe ya mkono 1,500,000 na plau 10,000 za kukokotwa na maksai kwa mwaka. Aidha, mwaka huo huo mradi wa Zana za Kilimo wa Morogoro (The Morogoro Mechanization Project) ulianzishwa ambapo matrekta 150 aina ya FIAT yaliingizwa na kukopeshwa kwa wakulima, Serikali za Vijiji na Vyama vya Ushirika. Kati ya mwaka 1984 hadi 2001, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, iliwezesha upatikanaji wa matrekta 308 aina ya Kubota yaliingizwa nchini na kusambazwa kwa

Vyama vya Ushirika na wakulima binafsi katika mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya kuendeleza kilimo hasa cha zao la mpunga. Aidha, matrekta ya mkono 170 aina ya KUBOTA yalikopeshwa kwa nusu bei ya shilingi milioni 2.5 kwenye skimu za umwagiliaji Tanzania Bara.

Mwaka 1994, Serikali ilianzisha Mfuko wa Pembejeo za Kilimo kwa lengo la kutoa mikopo yenye riba na masharti nafuu kwa wakulima na wasambazaji wa pembejeo za kilimo na mifugo nchini. Aidha, mwaka 2003/2004 Mfuko ulianza utoaji wa mikopo ya matrekta mapya na viambata vyake, na ukarabati wa matrekta chakavu. Hadi mwaka 2025, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ulikuwa umetoa mikopo iliyowezesha wakulima kununua matrekta makubwa 1,260 na matrekta madogo 273 na viambata vyake. Kupitia Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani (*District Agricultural Development Plans*) chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP ) mwaka 2008/2009, Serikali ilianzisha utaratibu wa wakulima kuwezeshwa kupata zana za kilimo yakiwemo matrekta makubwa na madogo, na mashine za usindikaji kwa mpango wa ruzuku. Programu hiyo iliwezesha wakulima kupata matrekta madogo 3,562 na matrekta makubwa 169 kwa mpango huo wa ruzuku.

Mwaka 2009/2010 Serikali kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa - SUMA JKT iliingiza jumla ya matrekta 1,846 na viambata vyake, pampu za kusukuma maji 1,100 na matrekta madogo ya mkono (powertiller) 400. Mwaka 2014/2015, Serikali kupitia Mradi wa Sera na Maendeleo ya Rasilimali Watu (PHRD) ilinunua mashine za kuvuna mpunga (*rice combine harvesters*) 64, kupura mpunga (*threshers)* 36, kukata mpunga (reapers) 16 na mitambo midogo 14 ya kusindika mpunga na kuzisambaza mashine hizo kwenye skimu 14 za umwagiliaji. Aidha, katika vipindi tofauti Serikali imefuta Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa

Forodha kwa matrekta na zana nyingine za kilimo kwa lengo la kupunguza gharama za ununuzi wa zana za kilimo kwa wakulima.

### 1.4 Hali ilivyo sasa ya Matumizi ya Zana za Kilimo

Serikali imeendelea kuhimiza matumizi ya zana za kilimo pamoja na kutoa huduma za kitaalamu, ili kuongeza wigo wa matumizi ya zana za kilimo, kuendeleza teknolojia bora za umwagiliaji, kuongeza tija na kupunguza harubu katika uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo.

Kumekuwa na mabadiliko makubwa katika eneo la ukatuaji mashamba kwa kutumia zana za kisasa za kilimo hususan matrekta. Kwa mujibu wa Hotuba ya Bajeti Wizara ya Kilimo mwaka 2025/2026, idadi ya matrekta makubwa na matrekta madogo yamefikia 28,693 na 23,315 mtawalia. Hatua hiyo, imechangia ongezeko la matumizi ya matrekta nchini kutoka asilimia 25 mwaka 2023/2024 hadi asilimia 26 mwaka 2024/2025 sawa na wastani wa matumizi ya trekta moja kwa hekta 500. Pamoja na ongezeko hilo la matumizi ya matrekta, kazi nyingine za shamba katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji mazao kama vile kupanda, kupalilia, kunyunyuzia viuatilifu na kuvuna bado zinafanyika kwa kutumia nguvu ya binadamu. Hali hiyo inasababisha mkulima kutumia muda mwingi shambani lakini pia kuchangia upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno.

Aidha, usindikaji wa mazao nchini, hususan mpunga na mahindi umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 80 kutokana na matumizi ya mashine zikiwemo mashine za kukoboa na kusaga. Licha ya jitihada na mafanikio mbalimbali katika tasnia ya zana za kilimo bado tasnia hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo;

i. Uhaba wa teknolojia za kisasa;
ii. Bei kubwa za matrekta na viambata vyake;

iii. Kukosekana kwa mikopo ya kutosha au mikopo yenye masharti magumu kwa wakulima;
iv. Uelewa mdogo wa matumizi ya zana kwa wakulima na maopereta;
v. Uhaba wa utoaji wa huduma baada ya mauzo, mafundi na maopereta wa zana za kilimo;
vi. Upatikanaji usioridhisha wa vipuri na huduma za matengenezo hususan maeneo ya vijijini;
vii. Miundombinu duni mashambani inayosababisha zana za kilimo kutofanya kazi kwa ubora na ufanisi uliokusudiwa; na
viii. Ubora duni wa baadhi ya mashine kutoka nje ya nchi kuathiri uzalishaji wa ndani na kuwafanya wakulima kupata bidhaa zisizo za kudumu

## 1.5 Chimbuko la Mwongozo

Mwongozo huu unatokana na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya uwekezaji wa trekta 10,000 na trekta ndogo za mkono (powertillers) 800 ili kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa huduma za zana za kilimo katika mnyororo wa uzalishaji mazao kulingana na mahitaji ya wadau hususan wakulima wadogo. Kwa kutambua uwekezaji mkubwa wa zana za kilimo unaoendelea kufanywa na Serikali, Mwongozo huu ni nguzo muhimu sana kwani unatoa utaratibu wa matumizi endelevu ya uendeshaji wa vituo 1,000 vya Kata, Kanda na Taifa vya kutoa huduma za zana za kilimo na kuhakikisha jitihada zote zinazofanywa na serikali zinatekelezwa kwa ufanisi. Vilevile, Mwongozo unachochea kuongeza fursa za ajira kwa vijana na wanawake ambapo Sekta binafsi itashiriki kuanzisha karakana kwa ajili ya kutoa huduma za matengenezo, vipuri, mafuta na vilainishi.

Aidha, mwongozo huu ni sehemu ya utekelezaji wa Sera na mikakati mbalimbali ya Kitaifa inayolenga kuendeleza Sekta ya Kilimo ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa (2050), Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), Sera ya Umwagiliaji (2010), Mkakati wa Taifa wa Zana za Kilimo (2006), Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo Tanzania (2050), Ajenda 10/30 na Programu mbali mbali zinazotekelezwa na Wizara ya kilimo.

## 1.6 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu utatumiwa na wadau wote wanaohusika katika usimamizi, ukodishaji, uuzaji na watumiaji wa zana za kilimo. Wadau wa mwongozo huu ni Pamoja na Wizara ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha, Mashirika yasiyo ya kiserikali, Mashirika ya Msingi ya Kijamii, Mashirika ya Msingi ya Kiimani/Kidini, Vyombo vya habari, Vyama vya Ushirika, Taasisi za Fedha, watoa huduma binafsi na Wauzaji wa Zana za Kilimo. Wanufaika wa mwongozo wa kutoa huduma za zana za kilimo ni wakulima, vikundi vya wakulima, Vyama vya Ushirika, wafugaji na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

## 1.7 Malengo ya Mwongozo

### 1.7.1 Lengo Kuu

Kutoa utaratibu kwa wadau kuhusu usimamizi na uendeshaji wa vituo 1,000 vya Kata, Kanda na Taifa vya kutoa huduma za zana za kilimo kwa usawa, uwazi na kuwezesha matumizi yenye ufanisi na endelevu.

### 1.7.2 Malengo Mahsusi

i) Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya zana za kilimo ili kuhakikisha wakulima wanaongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo;
ii) Kuhamasisha usimamizi na matumizi endelevu ya zana za kilimo ambazo zitawezesha kilimo endelevu na kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu wa mazingira;
iii) Kuongeza tija katika kilimo kwa kuongeza matumizi ya zana katika mnyororo wa uzalishaji mazao ya kilimo
iv) Kuweka mfumo imara/madhubuti wa ufuatiliaji wa matumizi ya zana za kilimo katika vituo.

## 1.8 Mantiki ya Mwongozo

Tanzania inatambua umuhimu wa kujitosheleza kwa chakula, kupunguza umaskini na kuhakikisha usalama wa chakula nchini. Juhudi mbalimbali zinafanywa na Serikali ili kuongeza uwezo wa wakulima wadogo kutumia teknolojia na zana za kilimo kwa kuweka mazingira wezeshi ya Kisera na kimkakati. Mwongozo huu ni sehemu ya utekelezaji wa mikakati iliyoainishwa katika Taifa ambayo inajumuisha:- Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021; Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo Tanzania 2050. Sera ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi ya mwaka 2009 (*Public Private Partnership act of 2019)*; Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002; Mkakati wa Kuendeleza Zana za Kilimo wa mwaka 2006; na Mkakati wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2021-2026. Sera hizi, zimeainisha kushirikiana na Sekta binafsi kuhamasisha na kuendeleza matumizi endelevu ya zana za kilimo zinazozingatia kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira.

Kwa msingi huo, mwongozo huu umelenga kuanzisha na kuendeleza vituo vya zana za kilimo kwa ajili ya kuongeza matumizi bora ya zana za kilimo ili kuongeza tija na usalama wa chakula nchini pamoja na kupunguza umaskini. Aidha, Mwongozo huu utawezesha matumizi ya zana za kilimo kwa wakulima hususan wadogo pamoja na vijana na wanawake kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT).

## 2.0 UTARATIBU NA VIGEZO VYA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA ZANA ZA KILIMO KATIKA VITUO VYA SERIKALI

Serikali inaendelea kufanya uwekezaji mkubwa wa zana za kilimo kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wakulima ili kuongeza uzalishaji, tija na kuimarisha usalama wa chakula nchini. Kwa msingi huo, Wizara ya Kilimo inaendelea na uanzishaji wa vituo 1000 vya Kata, Kanda na Taifa vya kutoa huduma za zana za kilimo katika mikoa mbalimbali nchini. Sehemu hii ya Mwongozo huu, inaweka utaratibu na vigezo vya kutoa huduma za zana za kilimo katika vituo vilivyoanzishwa na vitakavyoanzishwa ili kuhakikisha vinatoa huduma iliyokusudiwa kwa njia endelevu.

### 2.1 Utaratibu wa Usimamizi wa Vituo vya Serikali

Wizara ya Kilimo ni msimamizi mkuu wa shughuli zote zinazotekelezwa katika vituo 1,000 vya Kata, Kanda na Taifa kutoa huduma za zana za kilimo kwa wakulima. Wizara itasimamia utekelezaji wa shughuli zote za vituo kwa ufanisi na utoaji wa huduma zenye ubora wa hali ya juu. Muundo wa usimamizi na mgawanyo wa majukumu umeainishwa kama ifuatavyo;

### 2.1.1 Muundo wa Usimamizi

Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Zana za Kilimo na Uongezaji Thamani itakuwa msimamizi mkuu wa vituo 1,000 vya Kata, Kanda na Taifa. Wizara itakasimu baadhi ya majukumu kwa Taasisi za Wizara, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia na kuendesha kazi za vituo husika. Taasisi za Wizara, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitateua wasimamizi watakao ratibu utekelezaji wa shughuli zote za utoaji huduma za zana za kilimo katika vituo. Lengo la muundo huu ni kuimarisha wajibu, uendelezaji na uendeshaji wa vituo ili kutoa huduma endelevu kwa wakulima nchini.

### 2.1.2 Mgawanyo wa Majukumu

Vituo hivi, vitaendeshwa kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali kuhudumia wakulima ambapo majukumu yao yameainishwa kama ifuatavyo;

## 2.2 Majukumu ya Wizara ya Kilimo

Msimamizi mkuu wa vituo 1,000 vya Kata, Kanda na Taifa vya kutoa huduma za zana za kilimo kwa wakulima nchini itakuwa na wajibu ufuatao;

i. Kununua zana za kilimo katika mnyororo wa uzalishaji mazao ya kilimo kwa ajili ya vituo;
ii. Kuanzisha Vituo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo vinavyokidhi mahitaji ya wakulima;
iii. Kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa vituo vya zana za kilimo vya Serikali vilivyo chini ya Taasisi za Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

iv. Kuwezesha upatikanaji wa watoa huduma za matengenezo, mafuta, vilainishi na vipuri kwa ajili ya zana za kilimo katika vituo;
v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli zote zinazofanywa na wasimamizi wa Vituo na watoa huduma;
vi. Kukasimu baadhi ya majukumu kwa Taasisi za Wizara, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia na kuendesha vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo;
vii. Kuandaa na kusambaza mikakati na miongozo ya zana za kilimo nchini na kufuatilia utekelezaji wake kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mita na wadau wengine;
viii. Kufanya mapitio ya Mwongozo ili kuendana na mahitaji ya wakati husika; na
ix. Kutatua migogoro baina ya wasimamizi Vituo na wakulima iliyoshindikana kutatuliwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 2.2.1 Majukumu ya Idara ya Zana za Kilimo na Uongezaji Thamani

Idara ya Zana za Kilimo na Uongezaji Thamani itakuwa na wajibu ufuatao katika kusimamia vituo 1000 vya Kata, Kanda na Taifa vya kutoa huduma za zana za kilimo nchini;

i. Kuteua mratibu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli zote zinazofanywa na wasimamizi wa Vituo na watoa huduma;
ii. Kuratibu na kusimamia shughuli zote za uendeshaji, utunzaji na uendelezaji wa Vituo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo kwa wakulima;

iii. Kuhakikisha zana za kilimo katika vituo vinapata huduma za matengenezo, mafuta, vilainishi na vipuri kwa wakati;
iv. Kutoa elimu ya kitaalamu kwa Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na wadau wengine juu ya uendeshaji, utunzaji, uendelezaji na matumizi sahihi ya zana za kilimo; na
v. Kutoa elimu kwa maopereta na wakulima kuhusu matumizi sahihi ya zana na umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kisasa katika kilimo.

### 2.2.2 Majuku ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

i. Kuteua Afisa Kiungo wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli zote zinazofanywa na wasimamizi wa Vituo na watoa huduma;
ii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli zote zinazofanywa na wasimamizi wa Vituo na watoa huduma katika Halmashauri na kutoa taarifa kwa Wizara ya Kilimo;
iii. Kuhakikisha Halmashauri za Wilaya zenye vituo, zinatoa taarifa za utekelezaji wa shughuli zote zinazofanywa na wasimamizi wa Vituo na watoa huduma;
iv. Kuhakikisha Halmashauri za Wilaya zinatoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo; na
v. Kutatua migogoro ya utoaji wa huduma za zana za kilimo kwa wakulima inayoweza kujitokeza katika ngazi ya Halmashauri.

### 2.2.3 Majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa

i. Kuteua Mtaalam Msimamizi wa uendeshaji na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Kituo/Vituo katika ngazi ya Kata;
ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli zote zinazofanywa na wasimamizi wa Vituo na watoa huduma katika ngazi ya Kata;
iii. Kuratibu upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo;
iv. Kuwachagua/kuwapata maopereta wenye sifa wa kuendesha zana za kilimo;
v. Kushirikiana na Wizara, kuhakikisha zana za kilimo katika vituo vinapata huduma za matengenezo, mafuta, vilainishi na vipuri kwa wakati;
vi. Kufuatilia na kutathmini maendeleo ya Vituo vya zana za kilimo na kutoa taarifa Ofisi za Mkoa na Wizara ya Kilimo; na
vii. Kutatua migogoro inayoweza kujitokeza baina ya watoa huduma wa zana za kilimo na wakulima.

### 2.2.4 Majukumu ya wasimamizi wa Vituo vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo

Wasimamizi wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo kwa wakulima watakuwa na wajibu ufuatao;

i. Kuandaa mpango kazi wa utoaji huduma za zana za kilimo kulingana na msimu wa kilimo wa eneo husika;
ii. Kutoa tangazo la kalenda ya kuanza kwa msimu wa kilimo kwa wakulima katika eneo husika;
iii. Kupokea maombi kabla ya msimu wa kilimo kuanza kutoka kwa mteja/wateja kwa mawasiliano rasmi (kujaza fomu ya maombi);

iv. Kusimamia zoezi la uchambuzi wa maombi kulingana na mahitaji ya mkulima/wakulima kabla ya kuanza kwa msimu wa kilimo;

v. Kufanya tathmini ya shamba la muombaji ikihusisha hali ya shamba, ukubwa wa shamba, mahali shamba lilipo na aina ya huduma;

vi. Kutoa taarifa mapema ya mapungufu na uwezekano wa kuyarekebisha kwa muombaji wa huduma za zana za kilimo ambao hawakukidhi vigezo;

vii. Kuainisha gharama za kutoa huduma kwa muombaji aliokidhi vigezo vya kupata huduma za zana za kilimo kabla ya kuanza kwa msimu wa kilimo;

viii. Kuhakiki stakabadhi za malipo kabla ya kutoa huduma;

ix. Kumjulisha muombaji na kumpa utaratibu wa kulipa gharama za kupata huduma kupitia akaunti ya Serikali;

x. Kuandaa ratiba ya utoaji huduma kwa wakulima kulingana na maombi yaliyowasilishwa katika kituo;

xi. Kutoa huduma husika kwa muombaji aliyokamilisha taratibu za malipo; na

xii. Kutoa ajira za muda kwa wafanyakazi wenye sifa, ujuzi na weledi kwa ajili ya uendeshaji wa zana za kilimo.

### 2.2.5 Vigezo vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo

Huduma za zana za kilimo zitatolewa kwa kuzingatia taratibu na vigezo vinavyohakikisha ufanisi, matumizi bora ya rasilimali na tija kwa wakulima. Msimamizi wa Kituo cha Zana za Kilimo ana jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za kituo kwa kufuata miongozo iliyopo, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha utunzaji wa zana na utoaji wa huduma bora. Wizara kupitia Idara ya Zana za Kilimo na Uongezaji Thamani itawajibika katka usimamizi, uratibu,

uendeshaji, utunzaji, Uendelezaji, kutoa mafunzo na ushauri kuhusu utekelezaji wa taratibu, hivyo kuwezesha vituo kufanya kazi kwa ufanisi na kuwa endelevu. Utambuzi, uteuzi na kipaumbele katika utoaji wa huduma za zana za kilimo utafanyika bila ubaguzi wa aina yoyote. Huduma hizi zitapatikana kwa watu wote bila kujali kabila, dini, jinsia, umri, uanachama wa kisiasa, hadhi au hali ya kijamii na kiuchumi.

### 2.2.6 Sifa za Waombaji wa Huduma za Zana za Kilimo

Huduma za zana za kilimo katika vituo hivi, zitatolewa kwa wakulima wenye sifa zifuatazo;

i. Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
ii. Awe amesajiliwa katika mfumo wa wakulima (farmers registration system) wa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za pembejeo za kilimo ikiwemo zana za kilimo;
iii. Awe anamiliki au amekodisha shamba la mazao ya kilimo ili kupata huduma za zana za kilimo;
iv. Awe na uwezo wa kulipa gharama kabla ya kupata huduma za zana za kilimo katika akaunti ya Serikali; na
v. Shamba lake liwe katika mazingira mazuri ili kuhakikisha zana zinafanya kazi kwa ufanisi.

### 2.2.7 Hali ya Shamba

Maeneo au mashamba ambayo huduma za zana za kilimo zinahitajika yanapaswa kuwa yamekaguliwa na kuandaliwa vizuri kabla ya huduma kutolewa. Eneo linatakiwa lisiwe na visiki, miamba, vifusi au vikwazo vingine vyovyote vinavyoweza kupelekea ugumu au kupunguza ufanisi katika utendaji kazi wa zana. Ukaguzi wa eneo au maeneo unapaswa kufanywa na mtaalam wa

zana za kilimo au/na opereta kabla ya kufanya uamuzi wa kutoa huduma katika eneo husika. Aidha, wakulima ambao watahitaji huduma ya kusafisha eneo jipya la kilimo watawasiliana na Msimamizi wa Kituo cha Zana za Kilimo ili wapewe ushauri wa kitaalam.

#### 2.2.8 Vyama vya Ushirika/Umoja/Vikundi vya Wakulima/Kampuni

Utoaji huduma za zana za kilimo katika vituo hivi, unatoa kipaumbele kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika na vikundi/umoja wa wakulima, hasa ambao wanalima mazao ya kimkakati. Aidha, wakulima wanaokidhi vigezo wenye mashamba makubwa na wenye maeneo madogo madogo waliokusanyika pamoja watapewa kipaumbele cha kupata huduma kwenye vituo kulingana na mahitaji yao ya uzalishaji wa mazao ya kilimo. Aidha, Vituo vitatoa huduma kwa kampuni zenye mashambwa makubwa yaliyokidhi vigezo na sifa za kupata huduma katika vituo vya Serikali.

#### 2.2.9 Modeli ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Serikali

Modeli hii, itahusisha Vituo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo vya Serikali vilivyopo chini ya Taasisi za Wizara ya Kilimo na Halmashauri za Wilaya ambapo zitatoa huduma kwa gharama nafuu, usawa na uwazi ili kuwezesha wakulima kupata huduma stahiki na vituo kuwa endelevu. Vituo vitakuwa vinatoa ajira za muda kwa wataalamu kulingana na mahitaji kwa ajili ya uendeshaji. Taasisi za Wizara na Halmashauri za Wilaya zitateua wasimamizi wa kusimamia na kuendesha vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo na kutoa taarifa kwa wadau kuhusu upatikanaji wa huduma za zana za kilimo. Wakulima watatuma maombi kwa kujaza fomu ya maombi (kiambatisho Na. 1) ya kupata huduma za zana za kilimo

kwa wasimamizi wa vituo ambapo watapewa utaratibu wa kupata huduma husika kulingana na mahitaji.

### 2.3 Majukumu ya Wadau Wengine

Mwongozo huu, utatekelezwa kwa kushirikisha wadau wengine ambao majukumu yao yameainishwa kama ifuatavyo;

#### 2.3.1 Ofisi ya Rais-TAMISEMI

i. Kuwa kiunganishi kati ya Wizara ya Kilimo na Halmashauri za Wilaya katika kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo katika ngazi za Halmashauri;
ii. Kusimamia Halmashauri za Wilaya zitoe elimu kwa jamii juu ya matumizi ya zana za kilimo;
iii. Kusimamia Halmashauri za Wilaya zitoe mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya zana za kilimo ili kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo;
iv. Kuwezesha upatikanaji wa miundombinu na huduma za kijamii kama vile barabara, maji na umeme.

#### 2.3.2 Wizara ya Fedha

i. Kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uwekezaji katika vituo vya zana za kilimo vya Serikali;
ii. Kuwezesha misamaha ya kodi kwa kuzingatia Sheria zilizopo kwa wadau wanaowekeza kwenye uanzishwaji wa Vituo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo kwa wakulima;
iii. Kuwezesha misamaha ya kodi kwenye vipuri vya zana za kilimo kwa kuzingatia Sheria zilizopo.

#### 2.3.3 Taasisi za Kifedha

i. Kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa wawekezaji kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha Vituo vya huduma za zana za kilimo;
ii. Kuimarisha dirisha la kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo zikiwemo zana za kilimo;
iii. Kutoa mikopo ya riba nafuu ya ununuzi wa zana za kilimo kwa ajili ya vituo vya kutoa huduma.

#### 2.3.4 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

i. Kuhamasisha wanachama wa Vyama vya Ushirika juu ya matumizi bora ya zana za kilimo;

ii. Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujenga na kuanzisha Vituo kwa ajili ya kutoa huduma za zana za kilimo;

iii. Kuratibu mahitaji ya matumizi ya zana za kilimo kwa wanachama na wakulima kupitia Vyama vya Ushirika;

iv. Kufanya upekuzi na kusimamia mikataba itakayoingiwa baina ya Vyama vya Ushirika na Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo;

v. Kuratibu upatikanaji wa taarifa sahihi juu ya matumizi ya zana za kilimo kupitia Vyama vya Ushirika.

#### 2.3.5 Sekta binafsi

i. Kutoa huduma ya kuuza na kusambaza zana, vipuri, vilainishi vilivyothibitishwa na mamlaka husika;

ii. Kushiriki kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Vituo na kutoa mapendekezo ya kuboresha huduma kulingana na tathmini;
iii. Kushirikiana na Wizara ya Kilimo, kuandaa na kuwezesha mafunzo kwa wafanyakazi wa Vituo na wakulima kuhusu matumizi na matengenezo ya zana za kilimo; na
iv. Kushiriki katika kuunda mifumo ya ufuatiliaji utendaji wa kazi wavituo.

### 2.3.6 Washirika wa Maendeleo

i. Kuwezesha misaada ya kiufundi na ufadhili wa uanzishwaji wa Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo;
ii. Kusaidia uendelezaji wa teknolojia za zana za kilimo kulingana na viwango vya kimataifa na kushirikisha uzoefu kutoka nchi wabobezi wa teknolojia hizo; na
iii. Kuwezesha ufadhili wa mafunzo kwa wakulima na wafanyakazi (staff) kuhusu matumizi ya zana za kilimo.

### 2.3.7 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)

Kwa mujibu wa mwongozo huu, CAMARTEC itatekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika sheria Namba 19 ya mwaka 1981 ikiwa ni pamoja na kufanya majaribio ya matumizi (performance test) ya mashine na zana za kilimo zinazotarajiwa kutumika katika kilimo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Majaribio yanayofanywa na

CAMARTEC yanakusudia kuhakikisha zana za kilimo zinafaa kutumika katika mazingira ya hapa nchini.

### 2.3.8 Vyombo vya Habari

i. Kushirikiana na wataalamu wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo ili kuandaa maudhui yatakayotumika kwenye vyombo mbalimbali vya habari kuhusu matumizi bora ya zana za kilimo;

ii. Kutangaza vipindi mbalimbali kuhusu huduma zitolewazo na vituo vya zana za kilimo kwa wadau mbalimbali;

iii. Kuandaa vipindi vya maswali na majibu baina ya wakulima, watunga sera na wataalamu wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo ili kuongeza wigo wa uelewa wa teknolojia hizo

iv. Kuongeza uelewa wa mchango wa matumizi ya zana za kilimo katika kuongeza uhakika wa chakula na kuchangia maendeleo ya Sekta ya kilimo.

## 3.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UENDESHAJI WA VITUO VYA ZANA ZA KILIMO

Wizara ya Kilimo ndiyo msimamizi mkuu wa Vituo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo kwa wakulima ambapo wasimamizi wa vituo wote watawajibika kwa Wizara katika shughuli zote zinazohusiana na usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa utoaji huduma za zana za kilimo. Ili kuhakikisha ufanisi wa usimamizi na uendeshaji wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo mambo yafuatayo yatazingatiwa; Muundo wa usimamizi, ukokotoaji mjengeko wa gharama za kutoa huduma, mchanganuo wa matumizi ya mapato, mchanganuo wa tathmini ya maendeleo ya Vituo,

ukaguzi wa zana, upatikanaji wa zana, matengenezo na matengenezo kinga (*service*), vipuri na vilainishi, usalama wa zana za kilimo, opareta wa zana za kilimo, uondoshaji wa zana za kilimo na utekelezaji wa mwongozo.

## 3.1 Ukokotoaji Mjengeko wa Gharama za Kutoa Huduma za Zana za Kilimo

Sehemu hii inaelezea mjengeko wa ukokotoaji wa bei za kutoa huduma za zana za kilimo kwa wakulima zinavyopatikana. Bei hizi zitatofautiana kwa kuzingatia gharama za mafuta ya dizeli, vilainishi, matengenezo, matunzo na posho ya opereta katika Mkoa husika. Kwa msingi huo, bei za ukodishaji wa zana za kilimo zitatofautiana kati ya eneo moja hadi jingine. Ukokotozi huu umewekwa kwa lengo la kuhakikisha huduma za zana za kilimo zinatolewa kwa uwazi na gharama nafuu. Mjengeko wa bei za utoaji wa huduma za zana za kilimo utakokotolewa kama ifuatavyo;

Gharama halisi ya kulima kwa ekari (NCP)= $[AFC/TA + (FC * FP + 0.05FP * FC + L + CMPS)]$

Gharama ghafi ya kulima (GCP) kwa ekari=NCP+MK (25%*NCP)

**Ufunguo;**

AFC – *Annual fixed costs* (*Gharama za kudumu za mwaka mfano Bima* )

TA – *Targeted acrage* (*Ukubwa wa shamba kwa ekari* )

FC - *Fuel consumption* (*Matumizi ya mafuta kwa ekari*)

FP – *Fuel price* (*Bei ya mafuta* )

*NCP-Net cost of ploughing (gharama halisi ya kulima kwa ekari)*

*GCP-Gross cost of ploughing (gharama ghafi ya kulima)*

*CMPS-Cost of Maintenance,Parts & Service (Gharama za matengenezo, vipuri na sevisi)*

MK – *Mark up* (*Gharama za matunzo na usimamizi (20%-25%)*)

L- *Labor cost (Gharama ya kumlipa opereta na msaidizi)*

*0.05 – Additional cost factor (gharama za ziada)*

***Muhimu***

i. *Aidha, gharama za shughuli nyingine za mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa mazao zitawekwa kulingana na utaratibu wa kituo na kazi husika.*
ii. *Mfano wa ukokotoaji gharama za kupata bei ya utoaji huduma za zana za kilimo imeambatishwa kwenye jedwali Na: 1 & 3.*

## 3.2 Mchanganuo wa Matumizi ya Mapato

Mapato yatakayopatikana kwenye huduma za zana za kilimo yatatumika kwa shughuli mbalimbali za kituo ikiwemo usimamizi wa kituo utakaosimamiwa na Wizara na baadhi ya Taasisi zake. Gharama hizi zitagawanywa kutoka kwenye gharama za matunzo na usimamizi (Mark up) ambapo imekadiriwa kuwa asilimia ishirini na tano ya gharama halisi ya kulima. Mchanganuo umegawanywa kama ifuatavyo:-

i. Gharama za uendeshaji wa kituo (matunzo) = 75% ya Mark up (mishahara ya wafanyakazi, umeme, maji, bima, mawasiliano n.k.)
ii. Gharama za usimamizi (Wizara) = 25% ya Mark up

### 3.3 Tathmini ya Maendeleo ya Vituo

Vituo vinatakiwa kuwa endelevu na vyenye tija, hivyo zana za kilimo mpya na viambata vyake zitakuwa zikinunuliwa ili kufidia zana zilizofikia muda wa mwisho wa matumizi (salvage value). Tathmini ya nadharia ya vituo vya zana imefanyika kwa kuzingatia idadi ya mashine za kilimo zinazotarajiwa kununuliwa na kukabidhiwa vituo husika. Mashine za kilimo zilizonunuliwa na zinazotarajiwa kununuliwa zimeainishwa hapo chini ambazo ni trekta kubwa, trekta za mikono *(power tillers)* na mashine za kuvuna *(combine harvester)*. Tathimini na makadirio ya mgawanyo wa mapato umeainishwa kupitia jedwali hapo chini:-

***Jedwali:*** *Tathmini ya Mapato na Uendelevu wa Vituo*

| Na | Aina ya mashine | Idadi | Mgawanyo wa mapato | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uendeshaji | Mafuta | Matengenezo | Faida |
| 01 | Matrekta | 10,000 | 217,005,000,000 | 180,000,000,000 | 54,500,000,000 | 135,451,500,000 |
| 02 | Matrekta ya mkono (power tiller) | 800 | 6,674,166,667 | 2,400,000,000 | 960,000,000 | 3,010,250,000 |
| JUMLA | | | 223,679,166,667 | 182,400,000,000 | 55,460,000,000 | 138,461,750,000 |

### 3.4 Ukaguzi wa Zana za Kilimo

Ukaguzi wa zana utafanywa na watalaam wenye fani/ujuzi husika au opareta kwa kuzingatia mambo yafuatayo;

i. Kukagua zana zote kabla na baada ya kufanya kazi ili kujiridhisha usalama na ubora wa zana husika;
ii. Kufanya usafi wa zana mara baada ya kazi;
iii. Kutoa taarifa kwa Msimamizi wa Kituo kuhusu mahitaji ya vilainishi, mafuta, sevisi na matengenezo pale inapohitajika;

iv. Kutumia mafuta na vilainishi vilivyoainishwa kutoka katika vituo vya mafuta vilivyoidhinishwa na Msimamizi wa Kituo; na
v. Kuweka kumbukumbu sahihi ya matumizi ya zana za kilimo kama vile aina ya zana, masaa ya kazi, mafuta yaliyotumika, vilainishi, idadi ya ekari na eneo la kazi.

## 3.5 Matengenezo na Matengenezo Kinga

Matengenezo na matengenezo kinga ya zana za kilimo yanatakiwa yazingatie mambo yafuatayo;

i. Matengenezo kinga (Service) yatafanyika kulingana na maelekezo ya mtengenezaji wa zana husika.
ii. Katika kipindi cha uangalizi, matengenezo ya zana yatafanywa na msambazaji wa zana husika kulingana na mkataba.
iii. Baada ya kipindi cha uangalizi kumalizika, matengenezo yoyote yatafanywa na mtoa huduma ya matengenezo aliyepewa kazi hiyo.
iv. Kuhakikisha kwamba zana zinatengenezwa na wataalam wenye sifa/kituo cha huduma kilichoidhinishwa.

## 3.6 Vipuri na Vilainishi

i. Kutumia vipuri na vilainishi halisi kutoka kwa wauzaji na wasambazaji wa zana husika.
ii. Kuwepo na akiba ya vipuri muhimu karibu ili kufanikisha matengenezo kwa haraka.

### 3.7 Usalama wa Zana za Kilimo

Vituo vya zana za kilimo vitahakikisha kwamba zana zinakuwa salama wakati wote. Kituo kinapaswa kuwa na nembo/alama kwenye zana kwa ajili ya utambulisho. Kituo kinapaswa kuwa na sehemu maalum ya kuhifadhi zana na vipuri.

### 3.8 Opareta wa Zana za Kilimo

Msimamizi wa Kituo atatoa ajira ya muda kwa maopereta wenye ujuzi na leseni ya uendeshaji wa zana za kilimo kutoka kwenye Taasisi zinazotambuliwa na Serikali. Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya itaratibu upatikanaji wa maoperata wa zana za kilimo na kada nyingine zitakazohitajika ili kuhakikisha kuna kuwa na uwazi katika zoezi hilo.

### 3.9 Uondoshaji wa Zana za Kilimo katika Vituo

Zana zinapotumika au kukaa kwa muda huchakaa na hivyo kushuka thamani. Msimamizi wa Kituo atatoa mapendekezo ya uondoshaji wa zana za kilimo katika kituo kwa sababu mbalimbali ikiwemo kupunguza gharama za uendeshaji wa zana husika wakati gharama ya kumiliki na kutumia zana inapoongezeka kila msimu wa kilimo. Zana za kilimo zikiwemo mashine za kuvuna, trekta ndogo za mikono, trekta kubwa na zana nyingine zitaondoshwa baada ya kumalizika kwa muda wa kutumia zana kiuchumi (economic lifespan) ili Kituo kiweze kununua zana mpya na kuuza za zamani pamoja na kukwepa gharama zitakazokuwa zinaongezeka iwapo zana chakavu zitaendelea kutumika katika uzalishaji. Zana hizo, zitaondoshwa kwa kufuata taratibu za uondoshaji mali za Serikali na ukokotoaji uchakavu kama inayopendekezwa katika mfano wa jedwali Na. 2 & 4.

## 4.0 MASUALA MTAMBUKA

### 4.1 Jinsia, Vijana, Wazee na Watu wenye Mahitaji Maalum

Wanaume, wanawake na vijana wanatambulika kuwa, wadau muhimu katika maendeleo ya Sekta ya Kilimo nchini. Utoaji wa huduma za zana za kilimo utazingata vikundi vya wakulima au mkulima mmoja mmoja katika jamii huku kipaumbele kikiwa ni kwa wakulima vijana, wanawake, wazee na watu wenye mahitaji maalum.

### 4.2 Mabadiliko ya Tabianchi na Utunzaji wa Mazingira

Matumizi ya zana za kilimo yatazingatia kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira. Wadau wote waelimishwe juu ya ulimaji unaozingatia uhifadhi wa mazingira hususan maeneo yenye miinuko. Utupaji na uhifadhi wa taka zinazozalishwa kutokana na mashine na zana (vilainishi, vichujio vya mafuta, matairi na sabuni za kusafisha zana) ufanyike kwa mujibu wa sheria na kanuni za mazingira zilizopo.

Wadau wote wanapaswa kuhimizwa kutumia Kilimo Hifadhi ambacho kinalenga kuongeza tija, kipato cha mkulima, usalama wa chakula, kutunza mazingira na kuongeza rutuba ya udongo. Kilimo Hifadhi ni teknolojia inayohimili mabadiliko ya tabia nchi na matumizi jumuishi ya rasilimali mbalimbali zikiwemo udongo, maji na baonuai. Nguzo zake kuu tatu ni kukatua udongo kidogo wakati wa kuandaa shamba, utumiaji wa mazao funika na kilimo mzunguko.

### 4.3 Utawala Bora

Utawala bora katika uendeshaji wa Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo, unazingatia kanuni za uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji wa wananchi, utawala wa sheria, na ufanisi katika utumiaji wa rasilimali za Vituo. Utawala bora katika uendeshaji wa Vituo

unalenga kuhakikisha kuwa taratibu zote za utoaji huduma za zana za kilimo zinafanyika kwa njia ya haki, ufanisi na kwa manufaa ya wakulima, wafugaji na wadau wengine.

## 5.0 UENDELEVU WA VITUO VYA KUTOA HUDUMA ZA ZANA ZA KILIMO

Katika kuhakikisha Vituo vya kutoa huduma ya zana za kilimo vinakuwa endelevu, Wizara itazingatia usimamzi wa rasilimali ikiwemo zana, kushirikisha jamii na kuwa na mipango ya muda mrefu. Hii ni pamoja na kuwekeza zana zinazofaa kwa eneo husika, kutoa mafunzo kwa waendeshaji na watumiaji, usimamizi wa fedha, huduma za matengenezo, mafuta na kuzingatia athari za mazingira ili kuhakikisha uendelevu wa Vituo vya zana za kilimo.

### 5.1 Usimamizi na Matengenezo ya Zana za Kilimo

Zana za kilimo zinahitaji usimamizi, matumizi sahihi, matunzo, matengenezo mazuri kama inavyoelekezwa na mtengenezaji. Mwongozo huu, unawaelekeza wasimamizi wa Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo kuhakikisha waendeshaji (maopereta) wanazingatia maelezo ya mwongozo wa mtengenezaji (manufacturer manual) yatakayosaidia kuwa na matumizi sahihi na endelevu ili zana za kilimo ziweze kufanya kazi kwa muda mrefu na uendeshaji wake uwe na tija na gharama nafuu.

Zana za kilimo kama mashine nyingine yoyote zinahitaji matengenezo, sevisi, ukarabati wa mara kwa mara kama inavyoelekezwa kwenye mwongozo wa mtengenezaji. Wasimamizi wa Vituo wanatakiwa kuzingatia ili kuongeza muda wa maisha ya zana za kilimo, ufanisi na utendaji mzuri wa kazi. Matengenezo yafanywe na mtu mwenye ujuzi na uzoefu wa aina ya zana husika na tatizo lililojitokeza. Msimamizi na opereta wanatakiwa kuzingatia maelekezo ya uendeshaji, utunzaji, marekebisho ya kila siku na ya

vipindi maalum kulingana na mwongozo wa mtengenezaji. Zana zote zilizo katika kipindi cha muda wa uangalizi (*Warranty*), msimamizi anatakiwa kuwasiliana na muuzaji au wakala wake aweze kufanya matengenezo kulingana na mkataba wa muda wa uangalizi (*Warranty*).

## 5.2 Upatikanaji wa mafuta na vilainishi *(lubricants)*

Kutakuwa na watoa huduma ya mafuta ya kuendeshea zana za kilimo na vilainishi (*lubricants*). Watoa huduma hizi watapatikana kupitia utaratibu wa manunuzi na watagawanyika kwenye Kanda mbalimbali. Watoa huduma watakuwa wanasambaza mafuta na vilainishi vya zana za kilimo kwenye vituo vya zana za kilimo pindi zitakapohitajika kwenye zana zote za kilimo zilizopo kwenye kanda husika.

## 5.3 Usimamizi wa Fedha na Mapato

Kwa mujibu wa mwongozo huu, Wizara ni msimamizi wa fedha na mapato yote yanayotokana na Vituo ilivyoanzisha. Wizara itahakikisha makusanyo na mgawanyo sahihi wa rasilimali kwa watoa huduma wote. Aidha matumizzi ya fedha yanapaswa kuendana na mpango wa mwongozo huu. Kuhakikisha matumizi ya fedha yanaendana na malengo ya kifedha na utekelezaji kwa kila kituo. Mapato yatakayopatikana itakuwa ni sehemu ya chanzo cha mapato cha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (*Agriculture Development Fund – ADF*), ambayo itagawanyika kwenye maeneo mbalimbali kama Uendeshaji (*Operation*), Matengenezo (*Maintenance*), mafuta (*Fuel*) na Faida (*Profit*). Miamala yote itakuwa kwa mujibu wa kanuni na miongozo ya kifedha iliyopo ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa akaunti ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na uendelevu wa shughuli za kituo. Usimamizi wa mapato uzingatie yafuatayo;

i. **Utoaji wa Huduma:** Kutoa huduma za zana kwa wakulima kwa kuzingatia gharama za uendeshaji za wakati husika kulingana na mjengeko wa bei ambao umewekwa na mwongozo huu. Hatua hiyo itawezesha vituo kujiendesha na kutoa huduma endelevu.

ii. **Ufuatiliaji wa Mapato:** Kuweka mfumo madhubuti wa kufuatilia na kutunza taarifa sahihi ya mapato yote yatokanayo na huduma zinazotolewa na kituo. Hii inajumuisha kutunza kumbukumbu za malipo, stakabadhi na taarifa za kifedha, pamoja na kuweka mifumo ya kidigitali ya ulipaji na ufuatiliaji wa mapato.

iii. **Matumizi ya Mapato:** Matumizi ya fedha yatazingatia sheria, taratibu, na miongozo ya matumizi ya fedha za Serikali. Matumizi hayo yatahusisha matengenezo ya zana; Kulipa watoa huduma wanaoendesha Vituo vya zana za kilimo na Kulipia huduma ya mafuta;

iv. **Akaunti ya fedha:** Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo utakuwa na akaunti ambayo itakusanya mapato yatokanayo na Vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo ambapo sehemu ya mapato itatengwa kwa ajili ya uwekezaji zaidi katika uboreshaji wa huduma za zana za kilimo. Hii inahakikisha ununuzi wa zana mpya na kuboresha miundombinu bila kutegemea msaada wa nje.

v. **Uwazi na Uwajibikaji:** Matumizi ya mapato yatazitangatia uwazi na uwajibikaji na kuhakikisha kuwa Vituo vya zana za kilimo vinatoa huduma kwa manufaa ya wadau wote. Kwa kufanya hivyo, tutajenga taifa imara lenye misingi imara ya maendeleo na utawala bora. Kwa kufanya hivyo, tutahakikisha kuwa rasilimali za Vituo zinatumika kwa njia bora na zinawanufaisha wadau wote kwa kutoa huduma bora na za msingi.

## 5.4 Kuratibu mafunzo na tafiti za zana za kilimo

Mafunzo na utafiti vitaratibiwa na Wizara ya Kilimo ikishirikiana na Taasisi na Idara zake ikiwemo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Idara inayosimamia Zana za Kilimo. Wizara kwa kushirikiana na wauzaji wa zana, VETA na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs) itawafikia wadau wa kilimo ili;

i. Kuhakikisha wataalamu wa uendeshaji na matengenezo ya zana za kilimo wanapewa mafunzo ya mara kwa mara kwa ajili ya kuboresha ujuzi wao.

ii. Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya zana na umuhimu wa teknolojia za kisasa katika kilimo.

## 5.5 Matumizi ya mifumo ya kidigitali

Mifumo ya kidigitali itatumika kwenye ufuatiliaji wa zana za kilimo (*tracking*), hii itarahisisha kutunza kumbukumbu sahihi ya maeneo yaliyohudumiwa ikiwa ni pamoja na matumizi ya dizeli, kujua muda wa sevisi utakapofika nk.

Mifumo ya kidigitali itatumika kuunganisha wakulima wanaohitaji huduma za zana na watoa huduma (*uberization*). Hii itaongeza upatikanaji wa masoko, ufanisi wa biashara na kupunguza gharama za ufuatiliaji na hivyo kuongeza mapato.

## 5.6 Ushirikishwaji wa jamii

Kushirikisha wakulima na wadau wengine katika mipango na uendeshaji wa kituo ili kuhakikisha kuwa kinakidhi mahitaji yao na wajione kuwa ni sehemu ya umiliki.

## 5.7 Huduma ya matengenezo na mfumo wa kidigitali

Kutakuwa na watoa huduma ya matengenezo ya zana za kilimo. Hawa watoa huduma watapatikana kupitia mchakato wa manunuzi na watagawanyika kwenye Kanda mbalimbali. Watatakiwa kutumia vipuri bora vinavyotolewa na mtengenezaji (manufacturer) wa zana au msambazaji. Watakuwa wanafanya matengenezo kwa zana zote kwenye vituo vilivyopo kwenye Kanda husika. Kutakuwa na mtoa huduma ya mifumo ya kidigitali kwa ajili ya ufuatiliaji wa zana za kilimo na kuwaunganisha watoa huduma na wanaohitaji huduma kama wakulima.

# 6.0 TARATIBU KWA VITUO VITAKAVYOENDESHWA NA WATOA HUDUMA BINAFSI

Wizara itaanzisha vituo vipya na kufufua vya zamani ambavyo baadhi vitakodishwa kwa watoa huduma binafsi ambao wanaweza kuwa watu binafsi, ushirika, kampuni binafsi, mashirika ya kidini na asasi za kiraia. Vituo hivi vitakodishwa kwa kufuata taratibu, kanuni na miongozo ya kisheria ili viwe na tija na uendelevu.

## 6.1 Modeli ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Sekta Binafsi

Mwongozo huu, unatambua umuhimu wa Sekta binafsi katika kuongeza na kuendeleza matumizi ya zana za kilimo nchini. Sekta binafsi inaendelea na utoaji wa huduma za zana za kilimo katika mnyororo wa uzalishaji mazao ya kilimo kwa wakulima ambapo modeli mbalimbali zinatumika zikiwemo Vyama vya Ushirika/umoja wa wakulima, mkulima binafsi na makampuni. Modeli hizi za sekta binafsi zinatoa huduma kwa kuzingatia miongozo na taratibu zao, ambazo mara nyingi hutegemea nguvu ya soko. Baadhi ya modeli hizo ni pamoja na;

### 6.1.1 Modeli ya ushirika/umoja wa wakulima

Modeli hii inajumuisha, Vyama vya Ushirika na vikundi vya wakulima vilivyosajiliwa ndani ya eneo maalum vinavyomiliki zana za kilimo na kuzisimamia kulingana na utaratibu waliojiwekea.

### 6.1.2 Modeli ya Mkulima binafsi

Kwenye modeli hii inatumika zaidi hapa nchini ambapo mkulima binafsi au wajasiriamali wadogo hadi wa kati, wenye kumiliki zana za kilimo, watatoa huduma za zana kwenye mashamba yao wenyewe na kukodisha kwa wakulima wengine kwa bei shindani ya soko.

### 6.1.3 Modeli ya Kampuni binafsi

Kwenye modeli hii, Kampuni zinazomiliki zana za kilimo katika mnyororo wa uzalishaji wa mazao ya kilimo zinatoa huduma kwa wakulima kulingana na mahitaji pamoja na taratibu za kampuni husika.

## 7.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Wizara kupitia Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini itafanya ufuatiliaji wa kina wa utekelezaji wa mwongozo na Vituo husika kwa ajili ya kujua ufanisi wa utendaji wa kazi, changamoto zilizopo na mipango ya kuendeleza vituo. Wasimamizi wa Vituo vya Serikali watawajibika kufanya ufuatiliaji wa kazi za kila siku na kuandaa taarifa itakayowasilishwa wizarani kwa utaratibu watakaoelekezwa. Tathmini ya ufanisi wa utendaji kazi ya vituo utafanyika mara mbili kwa mwaka na kuandaa taarifa ya kina.

## 8.0 MAPITIO YA MWONGOZO

Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitano ili kutoa muda wa kutosha wa utekelezaji na kubaini mahitaji ya maboresho kulingana na maoni ya watumiaji wa mwongozo. Hata hivyo, kutokana na taarifa ya Ufuatiliaji na Tathmini, mapitio ya mwongozo yanaweza kufanyika ndani ya mwaka mmoja ili kukidhi mabadiliko ya mahitaji ya teknolojia za zana za kilimo kwa wakulima na wadau wengine.

Kiambatisho Na. 1: Fomu ya taarifa ya maombi ya mkulima kupata huduma za zana za kilimo

**Taarifa za Mkulima**

i) Jina Kamili la Mkulima: ______________________________________

ii) Nambari ya Simu: ___________________________________________

iii) Mkoa: ___________________________________________

iv) Wilaya: ___________________________________________

v) Tarafa: ___________________________________________

vi) Kata: ___________________________________________

vii) Kijiji: ___________________________________________

**2. Taarifa za Shamba**

i) Ukubwa wa Eneo (kwa ekari): ________________________________

ii) Taja aina ya mazao unayolima ______________________________

iii) Mahali Shamba Lilipo (Kijiji, Kata, Tarafa):

iv) Umbali wa Shamba kutoka barabara kuu (km): _________________

**3. Huduma Inayohitajika**

(Tafadhali weka alama ✓ kwenye huduma unayohitaji)

☐ Kulima
☐ Kupiga haro
☐ Kupanda
☐ Kuweka mbolea kwa trekta

☐ Nyingine (tafadhali fafanua): ___________________________________

**4. Tarehe na muda unayohitaji kupata huduma:** _______________________________________________

**5. Maelezo ya Ziada (ikiwa yapo):**

Sahihi ya Mkulima: ________________________ Tarehe: ___________________

NB; Kumbuka: Tafadhali hakikisha unaweka taarifa sahihi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma unayoimba kwa wakati.

**Jedwali Na. 1:** Mfano wa ukokotoaji wa umri wa kiuchumi wa trekta kubwa

| Gharama kwa ekari= ((AFC / TA + (FC * FP + 0. 05FP * FC + L+CRPS)) + MK | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Gharama za kudumu za mwaka mfano Bima (*Annual Fixed Cost*(AFC)) | | | | | |
| Ukubwa wa shamba kwa ekari (*Targeted Acreage* (TH)) | | | | | |
| Matumizi ya mafuta (*Fuel Consumption* (FC)) | | | | | |
| Bei ya mafuta (*Fuel Price* (FP)) | | | | | |
| Gharama za matengenezo, vipuri na sevisi (*Repair, Parts and Service (*RPS)) | | | | | |
| Gharama ya kumlipa opereta na msaidizi (*Labour Cost* (LC)) | | | | | |


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Gharama za ziada (*Additional Cost Factor* (ACF)) | | | | | |
| Gharama ya kununua trekta | 55,000,000 | A | | | |
| Umri wa kiuchumi wa trekta | 5 | B | | | |
| Masaa ya kazi ya trekta | 5,000 | C | | | |
| Masaa ya matumizi ya mashine kwa mwaka | 1,000 | D | | | |
| Thamani ya mabaki mwisho wa umri wa kiuchumi | 11,000,000 | E=A/B | | | |
| Gharama ya upungufu wa thamani kwa mwaka | 8,800,000 | F | | | |
| Bima ndogo- (*Third party*) | 118,000 | G | | | |
| Bima kubwa – (*Comprehensive)* | 1,100,000 | H (Cost * 2%+VAT18%) | | | |
| Uhifadhi | 550,000 | I(1%*A) | | | |
| Matumizi ya mafuta kwa lita kwa saa L/h | 5 | J | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Gharama ya mafuta | 3,000 | K | | | |
| Upakaji mafuta/vilainishi | 450 | L (15% * K) | | | |
| Matengenezo na matunzo | 2,750,000 | M(5%*A) | | | |
| Gharama za mfumo wa ufuatiliaji (GPS) | 560,000 | P | | | |
| Gharama ya kudumu kwa saa | | | | | |
| Upungufu wa thamani | 7,333.33 | =(A-E)/C | | | |
| Bima | 98 | =G or H/D | | | |
| Uhifadhi | 69 | =1%*(A/C) | | | |
| Mfumo wa ufuatiliaji (digital cost) | 467 | =P/D | | | |
| Ada ya huduma ya mtandaoni | 117 | =25%*(P/D) | | | |
| Jumla ya gharama za kudumu kwa saa | ***8,084*** | | | | |
| Gharama zinazobadilika kwa saa | | | | | |
| Matumizi ya mafuta | 15,000 | =J*K | | | |
| Vilainishi | 2,250 | =L*J | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Matengenezo na matunzo | 2,292 | =M/D | | | |
| Posho ya opareta | 10,000 | | | | |
| Jumla ya gharama zinazobadilika | ***29,542*** | | | | |
| | | | | | |
| Faida (25%) | 11,287.63 | | | | |
| Gharama kwa ekari | **51,593** | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| Jumla ya gharama kwa saa/ekari | 396,867,500,000 | | | | |
| Faida (25%) | 119,060,250,000 | | | | |
| | | | | | |

**Jedwali na 2**. Mfano wa tathmini ya Uchakavu wa trekta kubwa kwa muda wa miaka mitano

| Mwaka | Thamani ya Awali (TZS) | *Depreciation* kwa Mwaka (TZS) | Thamani Iliyobaki Mwisho wa Mwaka (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | 55,000,000.00 | 8,800,000.00 | 46,200,000.00 |
| 2 | 46,200,000.00 | 8,800,000.00 | 37,400,000.00 |
| 3 | 37,400,000.00 | 8,800,000.00 | 28,600,000.00 |
| 4 | 28,600,000.00 | 8,800,000.00 | 19,800,000.00 |
| 5 | 19,800,000.00 | 8,800,000.00 | 11,000,000.00 |



**Jedwali Na. 3:** Mfano wa ukokotoaji wa umri wa kiuchumi wa trekta la mikono (Powertiller**)**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Gharama kwa ekari= ((AFC / TA + (FC * FP + 0. 05FP * FC + L+CRPS)) + MK | | | |
| Gharama za kudumu za mwaka mfano Bima (*Annual Fixed Cost*(AFC)) | | | |
| Ukubwa wa shamba kwa ekari (*Targeted Acreage* (TH)) | | | |
| Matumizi ya mafuta (*Fuel Consumption* (FC)) | | | |
| Bei ya mafuta (*Fuel Price* (FP)) | | | |
| Gharama za matengenezo, vipuri na sevisi (*Repair, Parts and Service (*RPS)) | | | |
| Gharama ya kumlipa opereta na msaidizi (*Labour Cost* (LC)) | | | |
| Gharama za ziada (*Additional Cost Factor* (ACF)) | | | |
| Cost of Power Tiller | | A | |


| | | | |
|---|---|---|---|
| Umri wa kiuchumi wa trekta | 3 | B | |
| Masaa ya kazi ya trekta | 1,500 | C | |
| Masaa ya matumizi ya mashine kwa mwaka | 500 | D | |
| Thamani ya mabaki mwisho wa umri wa kiuchumi | 5,000,000 | E=A/B | |
| Gharama ya upungufu wa thamani kwa mwaka | 3,333,333 | F | |
| Bima ndogo- (*Third party*) | - | G | |
| Bima kubwa (Comprehensive) | - | H (Cost*2%+VAT18%) | |
| Uhifadhi | 150,000 | I(1%*A) | |
| Matumizi ya mafuta kwa lita kwa saa L/h | | J | |
| Gharama ya mafuta | 3,000 | K | |
| Upakaji mafuta/vilainishi | 450 | L (15% * K) | |
| Matengenezo na matunzo | 750,000 | M(5%*A) | |
| Gharama ya kudumu kwa saa | | | |
| Upungufu wa thamani | 6,667 | =(A-E)/C | |
| Bima | - | =G or H/D | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Uhifadhi | 19 | =1%*(A/C) | |
| Jumla ya gharama za kudumu kwa saa | 6,685 | | |
| Gharama zinazobadilika kwa saa | | | |
| Matumizi ya mafuta | 4,500 | =J*K | |
| Vilainishi | 675 | =L*J | |
| Matengenezo na matunzo | 1,500 | =M/D | |
| Posho ya opareta | 10,000 | | |
| Jumla ya gharama zinazobadilika | 18,400 | | |
| Jumla ya gharama kwa saa/ekari | 25,085 | | |
| Faida (25%) | 7,526 | | |
| Gharama kwa ekari | 32,611 | | |
| Idadi ya matrekta | 800 | | |
| Idadi ya ekari | 500 | | |
| Jumla ya gharama kwa saa/ekari | 10,034,166,667 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Faida (25%) | 3,010,250,000 | | |
| Jumla ya Gharama ya kukodisha trekta kwa ekari | 13,044,416,667 | | |

**Jedwali na 4**. Mfano wa tathmini ya uchakavu wa trekta la mikono kwa muda wa miaka mitano

| Mwaka | Thamani ya Awali (TZS) | Depreciation ya Mwaka (TZS) | Thamani Iliyosalia Mwisho wa Mwaka (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | 15,000,000 | 2,700,000 | 12,300,000 |
| 2 | 12,300,000 | 2,700,000 | 9,600,000 |
| 3 | 9,600,000 | 2,700,000 | 6,900,000 |
| 4 | 6,900,000 | 2,700,000 | 4,200,000 |
| 5 | 4,200,000 | 2,700,000 | 1,500,000 |


Thamani ya Awali vs Uchakavu wa Trekta la Mkono kwa Mwaka
Thamani fedha kwa mwaka (TShs)
16,000,000
14,000,000
12,000,000
10,000,000
8,000,000
6,000,000
4,000,000
2,000,000
0
0
1
2
3
4
5
6
Miaka




Kwa maelezo zaidi wasiliana na Wizara ya Kilimo

Mji wa Serikali Mtumba,
S.L.P 2182,
**DODOMA**
Simu: +255 (026) 2321407
Email: ps@kilimo.go.tz